# CHRISTIAN SOCIAL SERVICES COMMISSION (CSSC)
# NORTHERN ZONE JOINT EXAMINATIONS SYNDICATE (NZ-JES)

# FORM SIX PRE-NATIONAL EXAMINATIONS 2026
# 121/2 KISWAHILI 2
## RASIMU / MWONGOZO WA USAHISHAJI

1. Aoneshe mchango wa fasihi simulizi katika fasihi andishi
   - Wahusika, fasihi simulizi inawahusika wanyama ambao hupatikana katika fasihi andishi mfano tamthiliya ya mashetani kuna wahusika kama shetani.
   - Matumizi ya ngoma na nyimbo katika fasihi andishi mfano katika tamthiliya ya nguzo mama.
   - Mtindo wa masimulizi katika fasihi andishi kwa mfano katika tamthiliya ya kilio chetu.
   - Mandhari, fasihi andishi hutumia mandhari yanayotumiwa na fasihi simulizi mfano katika riwaya ya janga sugu la wazawa imetumia mandhari ya ziwani.
   - Dhamira, dhamira zilizopo katika fasihi simulizi hupatikana pia katika fasihi andishi.
   - Matumizi ya vipera vya semi, fasihi andishi inatumia vipera vya semi kama vile methali, nahau n.k

   Hoja 5×2=10

2. Mwanafunzi aoneshe jinsi mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanavyobadili uhifadhi wa fasihi simulizi
   - Kutokana na ugunduzi wa maandishi umesababisha mabadiliko katika uhifadhi wa fasihi simulizi kutoka kichwani kwenda kwenye maandishi. Mfano hadithi za watoto huhifadhiwa kitabu.
   - Ugunduzi wa vifaa vya kunasia sauti, kama vile redio, simu, umesababisha fasihi simulizi kuhifadhiwa humo. Mfano michezo ya futuhi.
   - Ugunduzi wa sinema na mikanda ya video nayo imebadili uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi. Mfano nyimbo na michezo ya kuigiza.
   - Ugunduzi wa komputa nao umesababisha mabadiliko ya uhifadhi wa fasihi simulizi
   - Masuala ya mitandao ya kijamii nayo yamebadilisha uhifadhi wa fasihi simulizi kwa mfano nyimbo za muziki na injili zinahifadhiwa facebook, kwenye tovuti n.k.

   Hoja 5×2=10

3. Mwanafunzi afafanue aina za tamthiliya na mifano yake kama ifuatavyo
   - Tamthiliya za kihistoria. Mfano mkwawa wa uhehe na kinjekitile
   - Tamthiliya ya Melodrama hizi huishia na furaha. Mfano mabepari wa Venis.
   - Tamthiliya komedia hizi huchekesha. Mfano
   - Tamthiliya simanzi/trejedia/tanzia hizi huwa na hudhuni. Mfano kifo kisimani
   - Tamthiliya tredikomedia huwa na hudhuni lakini huwasilishwa kwa njia ya kuchekesha.
   - Tamthiliya bubu hizi huwa za ishara. Mfano tamthiliya za Mr. Bin
   - Tamthiliya Ramsa mfano futuhi, mfalme Juha.
   - Tamthiliya ya majaribio. Mfano jogoo kijijini

Alama 5×2=10

4. Mwanafunzi aoneshe mbinu za kifani zilizotumika
   - Muundo wa moja kwa moja umetumika
   - Mtindo wa masimulizi
   - Mandhari yaliyotumika sehemu yoyote ile ambapo wanatu wanaweza kukaa na kuzungumza. Mfano njiani, barabarani.
   - Wahusika, msimuliaji
     baba Adam na mama Adam na Ikram
   - Matumizi ya lugha
     Habari imetumia lugha nyepesi inayoelewekana yenye tamathali za semi. mfano sitiari, tashibiha, mdokezo na tashihisi.

Alama 5×2=10

5. Mwanafunzi aoneshe mandhari yaliyotumika katika diwani mbili alizosoma
   - Chungu Tamu
     - Mandhari ya nyumbani kwa chatu kuonyesha dhuruma.
     - Mandhari ya Uganda na Tanzania kuonesha athari za vita.
     - Mandhari ya manzese kuonesha umaskini
     - Mandhari ya Ostabei
     - Mandhari ya mahakamani kuonesha usaliti
   - Kimbunga
     - Mandhari ya Afrika kuonesha uongozi mbaya
     - Mandhari ya shambani kuonesha usaliti
     - Mandhari ya Zanzibar kuonesha kupiga vita madawa ya kulevya
     - Mandhari ya jikoni kuonesha wizi
     - Mandhari ya barabarani kuonesha kuendesha gari kwa umakini
     - Mandhari ya porini kuonesha usaliti
   - Fungate ya uhuru
     - Mandhari ya Afrika uongozi mbaya
     - Mandhari ya kanisani wizi
     - Mandhari ya msikitini wizi
     - Mandhari ya hospital uoga wa viongozi

**NB:** Mwanafunzi ataje na shairi

Utangulizi Alama 02

Hoja Alama 8×2=16

Hitimisho Alama 02 Jumla alama 20

6. Mwanafunzi aoneshe dhima za watunzi wa ushairi kwa kutumia diwani mbili alizosoma
   - Kimbunga
     - Kupiga vita usaliti shairi la kibwangai, madanganyano.
     - Kupiga vita wizi na udokozi shairi la paka
     - Kupiga vita rushwa shairi la rushwa
     - Kupiga vita uongozi mbaya shiri la Kimbuga, wenye vyao hawatubani
     - Kupiga vita utumiaji wa madawa ya kulevya shairi la vijana wa Zanzibar, na mnapata kitu gani
   - Chunga tamu
     - Kupiga vita, vita na uhasama shairi la daktari askari, tishio la binadamu
     - Kupiga vita dhuluma na unyonyaji shairi la chatu na kuku
     - Kupiga vita matabaka shairi la manzese mpaka ostabei, Thomas na Dotto
     - Kupiga vita usaliti shairi la fikra za waungwana
     - Kupiga vita uongozi mbaya shairi la wimbo wake hotubani
   - Fungate ya uhuru
     - Kupiga vita uongozi mbaya
     - Kupiga vita wizi
     - Kupiga vita rushwa
     - Kupiga vita matabaka

   NB: Mwanafunzi anaweza kuandika hoja nyingine zinazoendana na hizo hapo.

   Utangulizi Alama 01
   Hoja Alama $6 \times 3 = 18$
   Hitimisho Alama 01 Jumla alama 20

7. Mwanafunzi aoneshe jinsi uhuru unavyoweza kusababisha madhara katika jamii
   - Vuta n'kuvute
     - Kuwa na wanaume wengi mf. Yasmini
     - Kuzaa nje ya ndoa mf. Yasmini
     - Kuweka watu utawani mf. Shihab (Mume wa Yasmini)
     - Kukamata watu ovyo mf. Koplo Matata
     - Ulevi kupindukia mf. Denge na wenzake
   - Mfadhili
     - Usaliti mf. Dania
     - Uhujumu uchumi

- Kutokuwajibika
- Ulevi na uzembe kazini mf. Dania na Gaddi
- Uzinzi na umalaya Mf. Nyambuja

Utangulizi Alama 02

Hoja Alama 8×2=16

Hitimisho Alama 02 Jumla alama 20

8. Mwanafunzi aoneshe fikra zenye kuleta mabadiliko kama ifuatavyo:-
   - Kivuli kinaishi
     - Fikra za Mtolewa za kuondoa uongozi mbaya
     - Fikra za Bi kizee za kuondoa utendaji mbovu.
     - Fikra za wari za kukubali mabadiliko
     - Fikra za kupiga vita rushwa
     - Fikra za Mtolewa za kujitoa mhanga
     - Fikra za wanaginingi za kuwa na umoja na mshikamano
   - Morani
     - Fikra za Dongo za kujitoa mhanga
     - Fikra za Jalia na Dongo za kupiga vita uhujumu uchumi
     - Fikra za Jalia za kukataa rushwa
     - Fikra za Maputo na Malongo za kuhimiza umoja na mshikamano
   - Nguzo mama
     - Fikra za Bi Tano za kuondoa uzembe
     - Fikra za Bi nne kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii.
     - Fikra za Bi nane kuhusu kuleta haki na usawa katika jamii.

   NB: Mwanafunzi atoe hoja nyingine zinazoendana na hizo

   - Utangulizi atoe maana ya tafsiri Alama 02
   - Hoja Alama 8×2=16
   - Hitimisho Alama 02 Jumla alama 20